# Mchango wa Kiswahili katika Upunguzaji wa Ajali za Vyombo vya Moto Barabarani: Mifano kutoka Madereva wa Magari na Pikipiki Tanzania

Joseph Hokororo Ismail, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, P. O. Box 20, Lushoto, Tanzania (Barua pepe: jihokororo@yahoo.com)

## Ikisiri

*Makala haya yanajadili mchango wa Kiswahili katika kupunguza ajali za vyombo vya moto barabarani. Tangu serikali ya Tanzania iboreshe miundombinu ya barabra baada ya uhuru, mwaka 1961, kwa kutengeneza barabara zenye upana wa kutosha na ubora wake,ilitegemewa kwamba kutakuwa na upungufu ama uondoshwaji kabisa wa ajali za barabarani. Kinyume chake, na kama inavyoonekana kwenye vyombo mbalimbali vya habari, hata baadhi ya wa-Tanzania wamekuwa wamepoteza maisha kwa ajili ya ajali za mara kwa mara. Baadhi ya sababu zilizotolewa na mamlaka husika ni pamoja na mwendokasi wa madereva, uchakavu wa magari (vyombo hivyo), kukosa umahiri wa uendeshaji na hoja zinazohusiana na hizo. Waandishi na wataalam hawajaangazia namna matumizi ya lugha ya maelekezo yanavyoweza kuchangia katika kupunguza ajali za barabarani ambazo hupunguza nguvu kazi ya taifa lile liwalo. Madereva wa vyombo vya moto Tanzania hutumia lugha kuu mbili za mawasiliano wanapoendesha vyombo hivi yaani Kiingereza kwa madereva wachache sana na Kiswahili kwa madereva wengi. Lengo la makala haya ni kuonesha kwamba Kiswahili kina mchango mkubwa katika upunguzaji wa ajali barabarani hasa kwa kuangalia lugha za maekelezo zinazotolewa barabarani kwa madereva na hata lugha ya kuelimisha madereva wa vyombo vya moto. Vibao na maelekezo yanayotolewa barabarani baadhi yake yapo kwenye lugha ya Kiingereza, lugha ambayo madereva wengi hawaifahamu wala kujua kilichoandikwa. Makala haya inaona kwamba mabango ya maelekezo haya, vitabu vya sheria za usalama barabarani na mafunzo na semina za muda mfupi na elekezi kwa madereva, zikitolewa kwa Kiswahili, zitachangia sana kupunguza ajali za barabarani. Makala imeangazia madereva wa magari na pikipiki kwa kuwa Watanzania wengi wanatumia vyombo hivi katika usafiri na shughuli za kila siku kuliko vyombo kama ndege, boti,treni na baikeli.*

**Maneno ya msingi:** Vyombo vya moto, mabango, vibao, Kiingereza, Kiswahili

## 1.0 UTANGULIZI

Ajali za barabarani ni moja ya changamoto kubwa zinazoyakabili mataifa mengi duniani. Changamoto hii imekuwa na athari nyingi kwa jamii ikiwemo za kijamii, kiuchumi, kiafya, na kimaendeleo. Kwa mujibu wa ripoti na tafiti mbalimbali za usalama barabarani, ajali za barabari ni moja ya chanzo kinachoongoza katika kusababisha majeraha, ulemavu, na vifo kwa wingi. Kwa upande wa Afrika Mashariki, idadi ya raia wanaopoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa kudumu inaongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na ajali za njia za usafiri. Kulingana na utafiti wa Shirika la Afya Duniani uliofanywa mwaka 2016, kwa wastani, watu watatu kati ya kila watu elfu kumi hupoteza maisha katika nchi za Afrika Mashariki. Uganda iliripotiwa kuwa ilikuwa inaongoza ikiwa na idadi kubwa zaidi ya wanaokufa kutokana na ajali hizo huku ikufuatiwa na Tanzania, Rwanda, Kenya na Burundi (www.voaswahili.com).

Kwa mujibu wa Takwimu za Hali ya Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani ya 2017 iliyotolewa na Jeshi la Polisi Tanzania (2018), katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2017, jumla ya matukio makubwa ya usalama barabarani yalipungua kwa asilimia 41.5 ambapo matukio 6,022 yaliripotiwa nchi nzima ikilinganishwa na matukio 10,297 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Licha ya upungufu huo, idadi hiyo inadhihirisha kuwa ajali za barabarani bado zinapoteza ndugu zetu na nguvu kazi ya taifa. Ripoti hiyo inabainisha kuwa ajali nyingi zaidi zilizotokana na sababu za kibinadamu zilichangia kwa 86.5%, ubovu wa vyombo vya usafiri ulichangia 7.7% na sababu za kimazingira zilichangia 5.9%. Sababu za kibinadamu ni pamoja na uendeshaji wa hatari, uzembe wa madereva na watumiaji wengine wa barabara, mwendo kasi, mifugo isiyochungwa, kulipita gari lingine bila uangalifu, na ulevi. Ubovu wa vyombo vya usafiri unajumuisha ubovu wa magari, hitilafu za taa za kuongozea magari barabarani; na sababu za kimazingira zinajumuisha moto, alama za michoro ya barabarani,vizuizi vya njia, ubovu wa barabara, na vivuko vya reli.

Wataalam wa maswala ya barabarani  wanasema kuwa ajali nyingi za barabarani zinaepukika. Ni kutokana na ukweli huu, Tanzania imekuwa ikijitahidi kwa hali na mali kukabiliana na tatizo hili. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha sheria ya usalama barabarani, kubadilishwa kwa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na mabaraza ya ngazi ya mkoa nchini Tanzania (kila mamlaka zinapobaini kuwapo kwa uzembe na umuhimu wa hatua hiyo). Hatua nyiingine ni kama

ongezeko la faini kwa wakiukaji wa sheria za barabarani. Hivi karibuni imeshuhudiwa madereva wa mabasi ya mijini wakitakiwa kuwa na umri wa miaka 25 hadi 60, madareva wa mabasi ya shule na yanayosafiri masafa marefu wakitakiwa kuwa na umri wa kati ya miaka 30 na 60, na yeyote atakayeendesha zaidi ya saa nane kutakiwa kuwa na msaidizi. Kama hiyo haitoshi, imeshuhudiwa katika mkoa wa Mbeya, serikali ikiwaalika watu wa imani zote kwa ajili ya kuombea janga la ajali za mara kwa mara mkoani humo. Hizi ni dalili kwamba tunaanza kulivulia kofia tatizo hili ndio maana tumelipeleka kwenye mtazamo wa kidhanifu (kiimani) kuliko kisayansi.

Kwa ujumla, ingawa nchi yetu ina taasisi na vyombo vingi vinavyohusika kwa njia moja au nyingine na usalama barabarani, kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Usafiri wa nchi kavu na Majini, Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto, Wakala wa Barabara Tanzania, Wizara ya Mambo za Ndani, na ya Ujenzi na Mawasiliano, tatizo la ajali za barabarani limeendelea kuwa tatizo sugu. Hii inapelekea wito wa tafiti mbalimbali kuendelea kufanyika. Hata hivyo, ipo haja ya kulitazama tatizo mbali zaidi ya miundombinu, mwendo kasi, uzembe, ubovu wa vyombo vya usafiri, na sababu za kimazingira. Ni kwa sababu hii, makala haya yanaangazia mchango wa Kiswahili katika upunguzaji wa ajali za vyombo vya moto barabarani hususani kutoka kwa madereva wa magari na pikipiki nchini Tanzania. Matokeo ya utafiti huu yanakusudiwa kuwa na umuhimu mkubwa kwa wana-lugha pamoja na mamlaka za usafiri kutokana na masuala yaliyoibuliwa na mtafiti, mathalani kupitia kuibuliwa kwa sababu nyingine ya matumizi ya lugha za kigeni inavyochangia katika kuchochea tatizo hili, pia kupitia mapendekezo yaliyotolewa na utafiti huu.

**Malengo ya Utafiti**

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza mchango wa Kiswahili katika upunguzaji wa ajali za vyombo vya moto barabarani hususani kutoka kwa madereva wa magari na pikipiki nchini Tanzania.

Ili kufikia lengo kuu, utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi yafuatayo:

i. Kufahamu mtazamo wa madereva wa magari na pikipiki juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwenye alama za barabarani nchini Tanzania.

ii. Kutathmini mtazamo wa madereva wa magari na pikipiki juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye alama za barabarani nchini Tanzania.
iii. Kutathmini mchango wa Kiswahili katika kupunguza ajali za vyombo vya moto barabarani nchini Tanzania.

## 2.0 MAPITIO YA MAANDIKO JARABATI

Ili kupata ulinganifu na kuongeza umakini wa utafiti huu, mtafiti alifanya mapitio katika machapisho yenye maandiko mbalimbali juu ya usalama barabarani kwa kiasi cha kutosha. Baadhi ya machapisho yaliyopitiwa ni kama ifuatavyo.

Han na wenzake (2010) walichunguza juu ya uelewa wa mambo ya usalama barabarani kwa wazungumzaji wa Kiingereza kama lugha yao ya kigeni nchini Australia. Msimamo wa watafiti hawa ni kwamba maarifa yoyote ya masuala ya usalama barabarani huanzia kwa madereva wanaojifunza kupitia kusoma machapisho mbalimbali kisha kuzingatia mambo yote ya usalama barabarani kulingana na uelewa wanaoupata. Mchakato huu hutawaliwa na mahusiano ya kijamii na utamaduni wa madereva wa jamii inayohusika kutegemeana na sera na maelekezo ya mamlaka za eneo husika. Kwa hivyo, lugha inachangia kwa kiasi kikubwa madereva kuelewa alama na mambo yote ya kuzingatia kwa usalama barabarani.

Akichunguza athari tabia za madereva kwa ajali za barabarani katika jiji la Tabuk nchini Saudi Arabia, Issa (2016) anaripoti kwamba takribani 87% ya madereva wa vyombo vya usafiri vilivyofanyiwa utafiti na waliosababisha ajali, wanaelewa alama za barabarani zilizoandikwa kwa lugha ya Kiarabu ilhali 52% pekee ndio wanaofahamu zile zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Issa anaamini kuwa kiwango kidogo cha majibu sahihi kuhusu alama na utaratibu wa usalama barabarani vinaashiria mafanikio duni ya shule au taasisi zinazotoa mafunzo ya udereva kwa hivyo taasisi hizo hazina budi kuboresha mfumo wake wa utoaji mafunzo husika.

Katika utafiti alioufanya Akyüz (2017) anadai kuwa mawasiliano miondoko (hususani ya alama) ni lugha inayofungamana na utamaduni wa jamii fulani kwa hivyo utambuzi, tafsiri pamoja na tathmini ya alama (ishara) husika hutofautiana kati ya jamii na jamii. Kutokana na ukweli huo, Akyüz anachukulia kujiingiza kwenye utamaduni wa kigeni ni sawa na kufahamu maneno ya

wimbo bila kujua mziki wake au kuujua mziki bila kujua mapigo. Anahitimisha kwa kusisitiza matumizi ya alama ambazo zina maana sawa kwa lugha zote.

Hammoudi na wenzake (2014) wanadai kuwa miradi na mikakati mingi ya masuala ya usalama barabarani vinajikita zaidi katika miundombinu na vyombo vyenyewe. Ni wataalamu wachache sana wanaojikita zaidi kwa watumiaji wa barabara. Ni kutokana na ukweli huo, wanahitimisha kwa kupendekeza uboreshwaji wa taarifa za usalama barabarani bila kuwasahau wageni wajapo huko Abu Dhabi. Waaidha, wanapendekeza vipimo vya vileo kwa madereva pamoja na kuhakikisha elimu inakuwa endelevu na si kuishiwa wakati wa kampeni maalum tu. Wanaongeza kwa kupendekeza elimu hiyo kuwalenga watoto, waenda kwa miguu na watumiaji wengine wa barabarani ikiwemo madereva chipukizi.

Krishnan na wenzake (2018), sambamba na yote yaliyobainika, wanapendekeza kuwa moja ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na tatizo la ajali za barabarani nchini India ni kutoa elimu kwa abiria na waenda kwa miguu. Elimu hiyo si budi ijumuishe sheria na taratibu za utumiaji wa barabara na hilo linawezekana kwa kutoa elimu kuanzia shuleni pamoja na kutumia mabango na njia za kielektroniki.

Katika utafiti uliofanywa na Jamson na wenzake (2005), huko New Zealand, ilibainika kwamba madereva waliopita kwenye alama zilizokuwa zimeandikwa kwa lugha moja ya kigeni (hususani kwenye kupunguza mwendo) walikuwa wazito kupunguza mwendo jambo linaloashiria kuwa alama au maelekezo yaliyoandikwa kwa lugha za kigeni huwapa tabu madereva kutafsiri hali inayowapelekea kupunguza mwendo wakiwa wameshafika eneo husika (wakiwa wameshavunja sheria). Hali ilikuwa tofauti kwa maeneo ambayo alama hizo hizo zilikuwa zimeandikwa kwa lugha mbili. Katika maeneo hayo, madereva walionekana kuwa watiifu kwa kufuata maelekezo kabla ya kuyafikia maeneo husika. Watafiti hao wanahitimisha kwa kupendekeza matumizi ya lugha mbili au zaidi katika uandishi wa alama na maelekezo ya alama za barabarani.

Kwa ujumla, baadhi ya watafiti, kama vile Han na wenzake (2010), Issa (2016), Akyüz (2017), Hammoudi na wenzake (2014), Krishnan na wenzake (2018), pamoja na Jamson na wenzake (2005), wanazitazama sababu ajali za barabarani kwa mtazamo tofauti na ripoti zingine. Wao wanaenda mbali zaidi kwa kubaini alama na maelekezo ya usalama wa barabara kwa kuzifungamisha na utamaduni wa kila jamii. Wengine wanaona mafanikio ya alama na

maelekezo hayo yanategemea sana uelewa wa walengwa hususani kutokana na kiwango chao cha umilisi katika lugha zinazotumika. Hata hivyo, suala la namna matumizi ya lugha ya maelekezo yanavyoweza kuchangia kupunguza ama kuongezeka kwa ajali za barabarani halijagusiwa kinagaubaga na waandishi au wataalam wengi. Ni kwa sababu hii, utafiti huu umejikita katika kuchunguza mchango wa Kiswahili katika upunguzaji wa ajali za vyombo vya moto barabarani hususani kutoka kwa madereva wa magari na pikipiki nchini Tanzania.

## 3.0 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo ili kueleza kiuchambuzi mitazamo na maoni ya madereva wa magari na pikipiki kama ilivyojidhihirisha katika taarifa zilizopatikana nyanjani. Kadhalika, katika utafiti huu, mtafiti alitumia mkabala changamano katika ukusanyaji na uchambuzi data. Mtafiti alitumia mtindo wa maelezo ili kueleza tatizo kwa uyakinifu pamoja na muundo wa kiidadi kupitia majedwali.

Kwa upande wa eneo la utafiti; utafiti huu ulifanyika Mkoani Mwanza, Wilaya ya Nyamagana Tanzania. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, wilaya ya Nyamagana inakadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao 363,452. Utafiti huu ulihusisha kata zote 13 za wilaya husika. Kata hizo ni pamoja na Luchelele, Buhongwa, Butimba, Igogo, Igoma, Isamilo, Mahina, Mbugani, Mirongo, Mkuyuni, Pamba, Nyamanoro, na Nyamagana.

Katika usampulishaji na walengwa, utafiti huu ulihusisha jumla ya washiriki 260 wakiwemo madareva wa pikipiki 10 kwa kila kata na madereva wa magari 10 kwa kila kata. Mtafiti alichagua makundi haya kulingana na muda wa utafiti na kwa kuwa walengwa ndio walikuwa na taarifa sahihi za matumizi ya lugha katika alama za barabarani. Kwa hivyo sampuli ya washiriki ilisampulishwa kwa kutumia mbinu ya kusudio.

**Kwa upande wa mbinu za kukusanyia data**, mtafiti alitumia mbinu ya usimulizi mahojiano ya vikundi kwa madereva wa pikipiki na mbinu ya usaili uliofanyika kwa kila dereva wa gari. Mbinu hizi ziliteuliwa kulingana na upatikanaji wa kila kundi pamoja na kupata taarifa za kina zaidi, kwa sababu watafitiwa wanaweza kuuliza maswali na mtafiti pia anakuwa na uhuru wa

kuuliza maswali zaidi ambayo ni vigumu kufanyika kwa kutumia mbinu nyingine kama vile ushuhudiaji, au hojaji.

### 4.0 UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

Taarifa za utafiti huu zilipatikana kutoka kwa watafitiwa 260 wakiwemo madereva 130 wa pikipiki na madereva 130 wa magari. Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano ya vikundi ili kupata taarifa kutoka kwa madereva 130 wa pikipiki. Mbinu hii ilifanyika katika vikundi 26 ikijumuisha vikundi viwili kwa kila kata. Mbinu nyingine iliyotumika ni mahojiano yaliyofanyika kwa kila dereva wa gari. Mbinu hii ilitumika kwa madereva 130 wa magari ambapo kila kata walihojiwa madereva 10 wa magari.

Kutokana na majibu ya utafiti huu, madereva wote wa pikipiki 130(50%) waliopitia mafunzo walikiri kuwa mafunzo husika waliyapata kwa lugha ya Kiswahili. Kwa upande wa madereva wa magari, madereva 123(43.7%) walidai kuwa walipata mafunzo kwa lugha ya Kiswahili; na madereva 8(6.3%) pekee ndio waliosema walipata mafunzo yao kwa lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza. Madereva wote walioshiriki katika utafiti huu walidai kuwa licha ya Kiswahili kutawala mafunzo ya usalama barabarani, mafunzo hayo hufanikiwa kwa kiwango kidogo sana kwa kuwa wakufunzi hulazimika kuchanganya Kiingereza na Kiswahili. Kutokana na hilo, walidai kuwa mara nyingi wanapata uelewa zaidi kwa kujisomea wenyewe au kupata uelewa zaidi kupitia uzoefu.

Mtafiti alihitaji kufahamu ikiwa mafunzo husika yalikuwa yanaeleweka kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Madereva wote waliopata mafunzo yao kwa lugha ya Kiswahili walisema kuwa kilichokuwa kinaelezwa kilikuwa kinaeleweka lakini kwa kuwa alama ambazo wanapaswa kuzifuata zipo katika Kiingereza, baada ya kusoma wanakuwa wanayakumbuka maelezo lakini alama zenyewe wanalazimika kuzikariri. Watafitiwa hao walisema kuwa masuala mengi wanayoyazingatia wanapokuwa barabarani yanatokana na uzoefu tu na juhudi binafsi baada ya kupatiwa mafunzo. Kwa hivyo, madereva wale wasio na juhudi binafsi katika kujifunza wanaambulia patupu.

**Lengo la 1: Mtazamo wa madereva juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwenye alama za barabarani**

Mtafiti alihitaji kufahamu kati ya alama au maelekezo yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza na yale yaliyoandikwa kwa Kiswahili ni zipi zinazoeleweka vizuri kwa madereva. Washiriki wote walishiriki katika kujadili suala hili. Majibu ya watafitiwa katika maeneo yote hayakuwa na tofauti kubwa sana. Miongoni mwa madereva wote, madereva 242 sawa na 93.1% walidai kuwa wanaelewa zaidi alama au malekezo ya usalama barabarani yaliyoandikwa kwa Kiswahili kuliko yaliyoandikwa kwa Kiingereza; na madereva 18 (6.9%) pekee ndio waliosema wanaelewa vizuri zaidi Kiingereza. Wakifafanua majibu yao, wale waliosema wanaelewa zaidi alama na maelekezo ya Kiswahili, baadhi yao walidai ni kwa sababu Kiswahili ndio lugha wanayoifahamu vizuri zaidi kwa hivyo ujumbe unaokusudiwa wanauelewa kwa urahisi zaidi ukilinganisha na Kiingereza.

Madereva wengine kati ya hao waliohojiwa walisema kuwa Kiswahili ni lugha rahisi kwao kwamba maneno ya Kiswahili hayana utata na yanakuwa na maana sawa na maneno halisi yaliyopo katika maelekezo husika. Walisema hii ni tofauti na maneno ya tungo za Kiingereza katika alama au maelekezo ya usalama barabarani. Baadhi ya mifano ya maneno iliyotolewa ni maneno kama vile "*Slow Down", "Keep Left",na "Construction Ahead"*. Katika madai yao walisema maneno hayo ya Kiingereza yanahitaji kukariri tafsiri zake barabarani kwa sababu maneno husika hayana maana za moja kwa moja. Msisitizo zaidi uliendelea kuwekwa kwenye suala la kuelewa kwa kukariri maana au tafsiri za alama husika na siubayana katika kuelewa.

Katika vikundi vya madareva wa pikipiki, baadhi ya madereva walisema kuwa matumizi ya maneno ya Kiingereza yanawapa wakati mgumu kukumbuka tafsiri kila wakati wawapo barabarani hivyo inapotokea mawazo yako mbali ni rahisi sana kujisahau. Katika vikundi vingine, kwa hoja hiyo hiyo, walisema kuwa kulingana na maelekezo ya lugha hizo kuwa katika maneno tata ya Kiingereza yanafikia hatua yaonekana ya kawaida wala hawayatilii maanani sana. Mifano ya maneno yanayoonekana ya kawaida ni kama vile:

a) *In* - Kuingia
b) *Out* - Kutoka
c) *No Entry* – Usiingilie Hapa (Hakuna Njia Kuingia)
d) *No Exit* – Usitokee Hapa (Hakuna Njia Kutoka)

Uwezo mdogo wa kumudu lugha ya Kiingereza huchangia ajali za barabarani.Hii inatokana na ukweli kwamba madereva wengi hawafahamu tafsiri au maana ya alama zilizoandaliwa kwa

lugha ya Kiingereza bila kuwa na tafsiri ya lugha ya Kiswahili. Tunaona mfano wa maelezo yaliyoandaliwa kwa Lugha ya Kiswahili katika kielelezo (1) hapa chini.

**Kielelezo 1: Mfano wa Kibao chenye Tangazo lisiloeleweka**




Katika kielelezo (1) hapo juu *keep left* na *overtaking* liliweza kufahamika na madereva wengi walihojiwa  lakini neno *unless* halikufahamika.

Kwa baadhi ya madereva wa magari, walidai alama zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza hazitiliwi maanani. Baadhi ya madereva hao walisema kuwa matumizi ya lugha ya Kiingereza hupelekea alama husika kuonekana kama mapambo ya barabarani tu kwa kuwa hayapewi uzito na madereva. Katika kielelezo (2) madereva 50 walioshiriki kujua matumizi yake na hata ikawa n mazoea ya kukiona cha kawaida wawapo barabarani.

**Kielelezo 2: Mfano wa Kibao chenye Alama zisizoeleweka**



Katika kielelezo (2) madereva kulikuwa na mkanganyiko wa maana ya alama hii kati ya madereva walihojiwa . Hii inaonesha kwamba suala la lugha alama na matumizi yake barabarani bado ni changamoto kubwa kwa madereva. Mfano zaidi ni alama zilizowachanganya madereva kuhusu matumizi yake ni kielelezo (3) hapa chini:

**Kielelezo 3: Mfano wa Kibao chenye Alama zinazochanganya**




Kadhalika, mtafiti alihitaji kufahamu kama madereva wanazielewa vema alama za barabarani. Walio wengi walisema wanafahamu vema alama chache lakini zilizo nyingi wanazisahau maana yake. Mmoja wa madereva hao alisema kuwa kunakuwa na ugumu kuelewa alama hizi zinapofundishwa kwa Kiswahili, jambo ambalo alidai linaleta mkanganyiko katika tafsiri zake. Wengine katika vikundi walidai ili alama husika zieleweke kwa urahisi si budi zifundishwe kwa

lugha ya Kiingereza na wengine walisema alama hizo zinapaswa kuwa kwa Kiswahili ili watumiaji wa barabara wazielewe moja kwa moja bila kukariri.

Aidha, mtafiti aliuliza kama kuna ajali za barabarani zinazotokea zikitokana na tatizo la lugha. Asilimia 90 ya washiriki wote walikubali kwamba suala la lugha linahusika kwa kiasi kikubwa kwa sababu kutokana na mkanganyiko wa lugha kuna alama zinatafsiriwa tofauti na inavyotakiwa. Kwa ufafanuzi wa ukweli wa jambo hilo ilibainika kuwa alama zilizo katika lugha ya Kiingereza huwafanya madereva wasiwe makini barabarani na wasitilie maanani malekezo husika. Washiriki hao walisema kuwa wakufunzi wao pia huonekana kukanganywa na tafsiri ya alama husika kwa Kiswahili. Kwa mfono kielelezo (4) kinachoonesha jinsi kibao kinavyotumia lugha mbili huku kukiwa na tafsiri yenye ukakasi au isiyokubalika.

**Kielelezo 4: Mfano wa kibao kioneshacho alama mkanganyiko  na Changamoto za Tafsiri**




Kama inavyonekana katika kielelezo (4) kuna lugha mbili Kiswahili **hakuna kupita** na Kiingereza *no overtaking*. Tukiangalia kwa makini matini ya lugha chanzi **hakuna kupita** tafsiri yake sahihi kwa lugha Kiingereza ya Kiingereza haiwezi kuwa *no overtaking*. Tafsiri ingeweza kuwa No passing au no crossing na nyingine zinazoelekeana na hizi. Alama zenyewe zilizo ambatana na tangazo hizo ( kielelezo 4) pia zinahitaji ueledi wa kutafsiri ya alama/picha.

Aidha, mtafiti alihitaji kufahamu kama madereva wanajisomea mambo ya usalama barabarani hususani alama na maelekezo. Majibu ya swali hili yalidhihirisha kuwa walio wengi hawajisomei masuala haya. Wakitoa sababu za kwa nini hawasomi, walidai kwamba matini za mambo ya usalama zilizo katika lugha wanayoimudu (Kiswahili) ni chache na zilizopo hazina maarifa wanayokuwa wakiyatafuta. Wale waliosema wanajisomea, walisema wanapenda kujisomea matini zilizoandikwa kwa Kiswahili tu. Hata hivyo, majadiliano ya hoja hii yalifikia hitimisho kwamba kiwango cha usomaji wa masuala ya barabarani ni kidogo sana kwa sababu matini za Kiswahili ni chache sana. Wengine walidai kwamba hata matini za Kiswahili hawazisomi sana kwa sababu wanaamini watakanganyika kwa kuwa alama zenyewe zipo katika Kiingereza hivyo hawaoni umuhimu wa kujisumbua kusoma Kiswahili. Mtafiti aliibua swali kwa washiriki wenye mtazamo huu kwa kuwaomba waeleze njia mbadala wanazotumia kuhakikisha kuwa wanapata maarifa ya usalama barabarani. Washiriki walidai kwamba wanaokolewa na maarifa wanayoyapata kutoka kwa wenzao.

Kwa lengo la kufahamu utoshelevu wa Kiingereza au Kiswahili katika kutimiza malengo ya usalama barabarani, mtafiti alihitaji kufahamu kwamba madereva wanapokuta alama za barabarani zimeandikwa kwa kutumia lugha mbili hutilia maanani lugha gani au hutii maelekezo husika baada ya kuona lugha gani. Majibu ya madereva wote yalibainisha kuwa waonapo alama za barabarani zikiwa zimeandikwa lugha zote mbili hujikita zaidi katika lugha ya Kiswahili na ndio huwapa ujumbe kwa haraka zaidi. Mfano wa kibao chenye maelekezo ya lugha mbili zinazofahamika na madereva wengi na wanaotilia maanani Kiswahilini kama kilezo (5) hapa chini:

**Kielelezo 5: Mfano wa Kibao chenye Alama ya Kikomo cha Mwendo**




Dereva anapoona kibao kama (5) ni rahisi kuona katazo la kikomo cha mwendo kilichoandikwa kwa Kiswahili kuwa ni (20) na hivyo kutozingatia neno hilohilo kama lilivyotafsiriwa katika Kiingereza.

Kwa lengo la kupata mapendekezo halisi kutoka nyanjani, mtafiti aliwapa nafasi washiriki wote wa utafiti huu, kutoa maoni yao mmoja mmoja. Washiriki 239(91.9%) walishauri alama zote za barabarani ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili na mafunzo yatolewe kwa Kiswahili. Washiriki 17(6.5%) walishauri lugha zote zitumike kwa kila alama na mafunzo yatolewe kulingana na ufahamu au umahiri wa lugha wa walengwa (wanaofunzwa). Na washiriki 4(1.5%) pekee ndio waliomba alama zote ziendelee kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza na mafunzo yatolewe kwa lugha hiyo. Washiriki waliopendekeza lugha ya Kiingereza walitakiwa kueleza njia mbadala kwa Watanzania wengi wasiojua kusoma (wasiojua) Kiingereza. Walidai kuwa serikali na jamii hawana budi kukazania Kiingereza kufundishwa ipasavyo katika shule za msingi na sekondari. Pia, washiriki hao walipendekeza utolewaji wa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumiaji wa barabara kwa kuwa wao wanaamini kuwa tatizo kuwa ni utolewaji wa mafunzo.

**Kielelezo 6: Mfano wa Kibao chenye Alama zinazoweza kutafsrika Kirahisi**





Kielelezo 7: ni Mfano wa alama zilizoandikwa kwa kiingereza na kiswahili zinazoonekana na zinazoeleweka kwa urahisi hata kwa dereva anayekutana nazo kwa mara ya kwanza




Kukanganya kwingine ni katika mazingira ambayo kibao kimoja kinakuwa na matangazo yanayowasilisha ujumbe wa aina mbili au zaidi kwa lugha mbili tofauti.Katika mazingira haya dereva hukuna ghafla kibao hiki na kukazia kusoma maneno ya kibao ya mwanzoni tuu bila kuzingatia kukisoma kibao chote. Turejee mfano wa kielelezo (8) hapa chini.

Kielelezo 8: Mfano wa alama maana zinazokanganya




Katika Kielelezo hiki kuna neno la Kiingereza *slow down round about ahead-100* ambayo imetafsiriwa kama **nenda polepole mzunguko wa barabara mbele 300m.** Tukiangalia kwa makini matini haya mawili tunaona kwamba kuna utofauti wa vipimo na mpangilio wa vipimo hivyo. Katika matini ya Kiingereza imetolewa kipimo 100m wakati katika matini ya Kiswahili imetolewa kipimo 300m. Hapa dereva humuiya vigumu kufamu kipimo sahihi katika maelekezo ya mawili (mita 100 au mita 300). Mtindo wa uandishi katika tafsiri kwa Kiswahili pia imechanganywa ama imetafsiriwa kisisi 300m katika Kiingereza inategemewa isomeke mita 300 katika Kiswahili. Hii inatokana mtafsiri kuwaza kwa Kiingereza na kuandika kwa Kiingereza kwa kutumia maneno ya Kiswahili. Hili ni tatizo na changamoto kwa mustkabali wa barabarani dhidi ya vyombo vya moto na Kiswahili kwa ujumla.

**Changamoto za Tafsiri**

Katika kuangalia swala la vibao barabarani yapo maswala mbalimbali yaliyojitokeza katika kutafsiri. Tatizo la kwanza ni ukosefu wa wataalamu wa watafsiri nyanja ya mawasiliano barabarani. Jambo hili hujionesha katika baadhi ya vibao vyenye tafsiri iliyofanywa na Mamlaka ya barabara Tanzania. Kwa mfano, kielelezo (8) inaweza kuchukuliwa kuwa tafsiri hii imefanywa na  Mamlaka ya Barabara Tanzania.

Tatizo la pili ugumu wa tafsiri na kupata istilahi oani/mbadala kati ya lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili.Tatizo hili hujionesha katika mazingira ambapo kuna vibao vyenye maneno ya Kiingereza yanayotatiza katika kutafsiri kama inavyojionesha katika mifano ya kielelezo 9 na kielelezo 10 hapa chini.

Kielelezo 9: Mfano wa kibao chenye maneno tatizi ya tafsiri



**Kielelezo 10:**




**Athari za matumizi ya lugha ya alama bila maneno**

Ajali nyingine za barabarani zinaweza kusababishwa na uwepo wa vibao vyenye lugha ya alama bila maelezo. Athari hii inatokana na dereva kutotambua maana ya alama husika ama wakati mwingine kupuuzia maelekezo ya alama hizo. Kwa mfano, katika kielelezo (11) kuna alama inayosemekana kuonesha katazo la barabara kuingia lakini dereva ameingia bamoja na kuwa kwa kibao hicho.

**Kielelezo 11: Alama Katazo na athari zake kwa Madereva**



**5. 0 Hitimisho**

Lengo la makala haya ilikuwa ni kuonesha mchango wa Kiswahili katika upunguzaji wa ajali barabarani hasa kwa kuangalia lugha za maekelezo zinazotolewa barabarani kwa madereva na hata lugha ya kuelimisha madereva wa vyombo vya moto.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ni dhahiri kwamba mafunzo ya masuala ya usalama barabarani yanafanikiwa kwa kiwango kidogo kutokana na matumizi ya lugha ya Kiingereza katika alama husika hivyo upataji maarifa husika kutingwa na changamoto ya lugha. Kutokana na hilo, ilibainika kuwa madereva wengi hawazijui vema alama za barabarani na wale wenye uelewa na matumizi ya barabara ni kutokana na juhudi binafsi nje ya mafunzo, maarifa wanayopeana pamoja na kupata uzoefu wa muda mrefu. Ingawa mafunzo yanatolewa kwa lugha ya Kiswahili, uhusiano wa ufafanuzi na alama husika unapungua hali inayopelekea madereva kulazimika kukariri alama badala ya kuzielewa.

Pia, ilibainika kuwa madereva wanaelewa kwa urahisi alama zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kama vile *"Nenda taratibu", "pita kushoto/kulia*" na nyinginezo. Kutokana na sababu kwamba Kiswahili ni lugha rahisi na inayoeleweka vema kwa Watanzania. Madereva wengi wanaelewa na kuzingatia zaidi alama na maelekezo yaliyoandikwa kwa Kiswahili kuliko Kiingereza. Hii ni kwa sababu maneno ya Kiingereza yanawapa wakati mgumu kukumbuka kila

wakati kabla ya kuelewa, hii hupelekea alama za lugha ya Kiingereza kusahaulika kwa urahisi na hivyo kutotiliwa maanani.

Kadhalika, ilibainika kuwa madereva walio wengi hawajisomei masuala ya usalama barabarani. Hii ni kutokana na sababu kwamba matini nyingi za usalama barabarani zipo kwa lugha wasiyoimudu (Kiingereza) na chache zilizopo haina mambo muhimu. Kama hiyo haitoshi, madereva wengi wanaamini matini zilizoandikwa kwa Kiswahili zinakanganya kwa kuwa alama wanazokutana nazo au wanazotakiwa kuzifuata zinakuwa hazijaandikwa kwa lugha waliyoisomea.

**6. 0 Mapendekezo**

Kwa kuzingatia majibu ya utafiti huu, inapendekezwa kuwa mabango ya maelekezo haya, vitabu vya sheria za usalama barabarani na mafunzo na semina za muda mfupi na elekezi kwa madereva, zikitolewe kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu ndio lugha inayoeleweka kwa urahisi kwa Watanzania walio wengi.

Aidha, alama za barabarani zinapaswa ziandikwe kwa lugha zote mbili (Kiswahili na Kiingereza) ili kurahisisha uelewa kwa madereva wote.Lakini lugha ya kiswahili inapaswa ianze na kufuatiwa na Kiingereza.Mapendekezo ya Alama za barabarani ambazo zinatumika sana Tanzania na ambazo zinaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili ni kama zifuatazo katika (12):

e) *Stop* – Simama
f) *Go* – Nenda
g) *Road Work Ahead* – Ujenzi Unaendelea Mbele
h) *Slow Down* – Nenda Taratibu/Punguza mwendo
i) *Zebra crossing* – Wavuka kwa Miguu
j) *Stop Police* – Kizuizi cha Polisi
k) *One way* – Njia Moja Tu
l) *Roundabout* – Njia Panda
m) *Get Ready* – Jianadae
n) *Bus Stop* - Kituo cha Mabasi
o) *Police – Accident* – Kizuizi Ajali Mbele

Alama zinazotumika ziandikwe kwa maneno ya lugha ya Kiswahili badala ya matumizi ya lugha ya alama. Kwa watafiti wajao, mtafiti anapendekeza utafiti mwingine ufanyike juu ya mchango wa Kiswahili katika udhibiti wa ajali za barabara kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji.

**MAREJELEO**

Akyüz, U. (2017). Visual Signs as a Cross-Cultural Language. *International Journal of Sciences and Research,* 73 (4) 170-179 April 2017.

Hammoudi, A., Karani, G. na Littlewood, J. (2014). Road Traffic Accidents among Drivers in Abu Dhabi, United Arab Emirates. *Journal of Traffic and Logistics Engineering,* 2(1), 7-12, March 2014.

Han, J., Singh, M., na Zhao, D. (2010). Road Safety Literacy for Speakers of English as a Foreign Language: Educating Novice Drivers for the Public's Health Safety. *Literacy & Numeracy Studies,* 18 (1) 2010.

Issa, Y. (2016). Effect of Driver's Personal Characteristics on Traffic Accidents in Tabuk City in Saudi Arabia. *Journal of Transport Literature,* 10(3), 25-29, Jul. 2016.

Jamson, S. L., Tate, F. N. na Jamson, A. H. (2005). Evaluating the Effects of Bilingual Traffic Signs on Driver Performance and Safety. *Ergonomics* 48(15) 1734 – 1748.

Jeshi la Polisi Tanzania. (2018). *Takwimu za Hali ya Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani Januari - Desemba 2017.* Dar es Salaam: Jeshi la Polisi Tanzania.

Krishnan, S. Geetha, K. na Basri, R. (2018). *Road Accidents and Road Safety Measures in Tamil Nadu: An Analysis.* Unpublished paper.

Han, J., Singh, M., na Zhao, D. (2010). Road Safety Literacy for Speakers of English as a Foreign Language: Educating novice drivers for the public's health safety. *Literacy & Numeracy Studies,* 18 (1) 2010.

Issa, Y. (2016). Effect of driver's personal characteristics on traffic accidents in Tabuk city in Saudi Arabia. *Journal of Transport Literature,* 10(3), 25-29, Jul. 2016.

Akyüz, U. (2017). Visual Signs as a Cross-Cultural Language. *International Journal of Sciences and Research,* 73 (4) 170-179 April 2017.

Hammoudi, A., Karani, G. na Littlewood, J. (2014). Road Traffic Accidents among Drivers in Abu Dhabi, United Arab Emirates. Journal of Traffic and Logistics Engineering, 2(1), 7-12, March 2014.

Krishnan, S. Geetha, K. na Basri, R. (2018). Road Accidents and Road Safety Measures in Tamil Nadu: An Analysis. Unpublished paper.

Jamson, S. L., Tate, F. N., na Jamson, A. H. (2005). Evaluating the Effects of Bilingual Traffic Signs on Driver Performance and Safety - Ergonomics 48(15) 1734 – 1748.

**Tovuti**

https://www.voaswahili.com/a/waziri-avunja-baraza-la-taifa-la-usalama-barabaranitanzania/4469231.html

https://www.voaswahili.com/p/6617.html

**Viambatisho**

**Kiambatisho A: Kielelezo cha Kibao Ya Kuonesha Mwendo**




**Kiambatisho B: Kielelezo cha Kibao, Kuonesha punguza mwendo ( kivuko cha watoto)**




**Kiambatisho C: Kielelezo cha Kibao, Kuonesha  simama (waenda kwa miguu wapite)**

